**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**BUNGE LA TANZANIA**

---

# TAARIFA YA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA NISHATI NA MADINI KUHUSU UTEKELEZAJI WA MAJUKUMU YA WIZARA YA NISHATI NA MADINI KWA MWAKA WA FEDHA 2016/2017 PAMOJA NA MAONI YA KAMATI KUHUSU MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI KWA MWAKA WA FEDHA 2017/2018

---

**Imetolewa chini ya Kanuni ya 99(9) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Januari, 2016**

**MEI, 2017**

# TAARIFA YA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA NISHATI NA MADINI KUHUSU UTEKELEZAJI WA MAJUKUMU YA WIZARA YA NISHATI NA MADINI KWA MWAKA WA FEDHA 2016/2017 PAMOJA NA MAONI YA KAMATIKUHUSU MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI KWA MWAKA WA FEDHA 2017/2018

## 1.0 UTANGULIZI

**Mheshimiwa Spika**, kwa mujibu wa Kanuni ya 99 (9) na Kanuni ya 117(11) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Januari, 2016, naomba kuwasilisha Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Nishati na Madini Kuhusu Utekelezaji wa Majukumu ya Wizara ya Nishati na Madini, kwa Mwaka wa Fedha 2016/2017, pamoja na Maoni ya Kamati kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi, kwa Mwaka wa Fedha 2017 /2018.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati ilifanya vikao kadhaa kwa lengo la kupokea na kuchambua Taarifa ya utekelezaji wa Bajeti ya Wizara, kwa Mwaka wa Fedha 2016/2017 na kuchambua Makadirio ya Mapato na Matumizi, kwa Mwaka wa Fedha 2017/2018. Sambamba na utekelezaji wa shughuli hiyo, Kamati pia ilifanya mambo yafuatayo:-

i) Ukaguzi wa baadhi ya Miradi ya Maendeleo iliyoidhinishiwa Fedha kwa Mwaka wa Fedha 2016/2017;
ii) Kupokea Taarifa ya Utekelezaji wa Bajeti pamoja na Maoni na Ushauri wa Kamati kwa Mwaka wa Fedha 2016/2017;

iii) Uchambuzi wa Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara kwa Mwaka wa Fedha 2017/2018.

**Mheshimiwa Spika**, Taarifa hii inaonesha matokeo ya shughuli hizo pamoja na Maoni na Ushauri wa Kamati.

## 2.0 UKAGUZI WA MIRADI YA MAENDELEO ILIYOTENGEWA FEDHA KWA MWAKA 2016/2017

**Mheshimiwa Spika,** kwa kuzingatia masharti ya Kanuni ya 98(1) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Januari, 2016, Kamati ilifanya ziara za ukaguzi wa Miradi ya Maendeleo inayotekelezwa chini ya Wizara ya Nishati na Madini, katika Mikoa ya Dar es Salaam, Tanga na Geita. Lengo la ziara hizo lilikuwa ni kujionea utekelezaji wa Bajeti ya Maendeleo iliyoidhinishwa kwa Mwaka wa Fedha 2016/2017 pamoja na changamoto zilizojitokeza katika utekelezaji wake.

Aidha, Kamati ilikagua Miradi iliyotengewa fedha na ambayo haikutengewa fedha katika Bajeti ya Maendeleo ya Mwaka 2016/2017 na miradi ambayo inatekelezwa katika Sekta ya Madini. Miradi iliyokaguliwa ni hii ifuatayo:-

i) Miradi ya Umeme Vijijini, Wilaya ya Tanga Vijijini;
ii) Miradi ya Umeme Vijijini, Wilaya ya Geita Vijijini;
iii) Mradi wa Umeme wa Gesi Kinyerezi I Extension (MW 185);

iv) Mradi wa Umeme wa Gesi Kinyerezi II (MW 240);

v) Ukarabati wa Kituo cha Kufua Umeme, Hale;

vi) Mradi wa Umeme Bulyanhulu-Geita KV 220;

vii) Mgodi wa Dhahabu wa Backleef;

viii) Migodi ya Wachimbaji Wadogo waliopata Ruzuku ya Serikali; na

ix) Migodi ya Wachimbaji wa Kati.

## 2.1 Maelezo na Matokeo ya Ukaguzi wa Miradi ya Maendeleo kwa Mwaka wa Fedha 2016/2017

### 2.1.1 Miradi ya Sekta ya Nishati iliyokaguliwa na Kamati

#### 2.1.1.1 Miradi ya REA katika Mkoa wa Tanga

**Mheshimiwa Spika**, katika Mkoa wa Tanga miradi ya umeme vijijini (REA) katika awamu ya kwanza na awamu ya pili, imetekelezwa katika wilaya nane (8) za mkoa huo. Miradi hiyo yenye ukubwa wa **KV 33** imetekelezwa na wakandarasi wawili ambao ni *STEG International Services Ltd* na Sengerema *Engineering Group Ltd*. Jumla ya vijiji **218** vya mkoa wa Tanga vimenufaika na ukamilishwaji wa miradi ya REA katika awamu ya pili.

**Mheshimiwa Spika,** ziara ya ukaguzi wa utekelezaji wa miradi hiyo ilifanyika katika Kijiji cha Tongoni, katika Wilaya ya Tanga Vijijini, ambacho ni kama kijiji cha mfano miongoni mwa vijiji vilivyopata umeme wa REA Awamu ya Pili.

Katika mradi huu Kamati yako ilibaini kuwa malengo ya mradi katika awamu ya pili, hayakukamilika kwa asilimia mia moja. Mradi ulilenga kuzipatia umeme kaya **138,** hata hivyo, ni kaya 90 tu kati ya hizo ndizo zimepata umeme, ambazo ni sawa na asilimia **65%** tu.

**Mheshimiwa Spika,** kwa upande mwingine, changamoto kubwa iliyobainika katika miradi ya REA katika Mkoa wa Tanga, ni pamoja na uunganishwaji mdogo wa Wananchi katika huduma hii ya nishati, Mashine Humba (Transformer) kuharibika mara kwa mara na kushindwa kukidhi mahitaji ya eneo husika.

Pia Kamati ilibaini kuwa, baadhi ya vitongoji na vijiji havijaunganishwa na huduma ya umeme katika awamu mbili zilizokwisha kamilika. Kwa maoni ya Wananchi ambao Kamati ilipata fursa ya kuzungumza nao waliieleza Kamati kuwa, tafiti (survey) zilizofanyika mwaka 2015 katika maeneo ya mradi hazikuwa za kimkakati *(not strategic)*kwa kuwa mchoro wa mradi husika ulisababisha nguzo za umeme kuwekwa katika maeneo ambayo wananchi walio wengi hawanufaiki.

Kwa upande mwingine, Kamati ilibaini kuwa, elimu kuhusu mradi wa ***densification*** kwa wananchi haikueleweka vizuri na

pia mradi husika haujaanza rasmi katika vijiji vyote ambavyo havikuunganishwa katika awamu zilizokwishakamilika.

**Mheshimiwa Spika,** napenda kulijulisha Bunge lako tukufu kwamba, kufuatia ziara ya Kamati katika Kijiji cha Tongoni, mashine Humba iliyokuwa na tatizo imebadilishwa, na Kamati inaipongeza sana Serikali kwa kuchukua hatua mapema.

#### 2.1.1.2 Miradi ya REA katika Mkoa wa Geita

**Mheshimiwa Spika,** Mkoa Geita umenufaika na Mradi wa Umeme Vijijini katika awamu ya pili, ambapo zaidi ya vijiji 101 vilivyokuwa kwenye tathmini ya awali vimeunganishwa. Mkandarasi aliyeshughulika na uunganishaji wa umeme katika Mkoa huu ni M/s Nakuroi Investment Co Ltd. Kamati ilifanya ukaguzi wa utekelezaji wa miradi hiyo katika vijiji vya Nyakato na Buzilayombo, kama vijiji vya mfano miongoni mwa vijiji vilivyopata umeme wa REA awamu ya pili.

Katika mahojiano na wananchi wa vijiji hivyo, Kamati ilibaini kuwa malengo ya mradi katika awamu ya pili ilikuwa ni kuzipatia umeme kaya 165 katika kijiji cha Buzilayombo na kaya 127 katika kijiji cha Nyakato. Hata hivyo, kati ya hizo, ni kaya 130 sawa na **asilimia 78%** zilikuwa zimepata umeme

katika kijiji cha Buzilayombo na kaya 32 sawa na **asilimia 25%** tu katika kijiji cha Nyakato.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati ilibaini kwamba, changamoto kubwa katika miradi ya REA inayotekelezwa katika Mkoa wa Geita ni uunganishwaji mdogo wa Wananchi katika huduma ya umeme na hivyo kutokufikiwa kwa malengo ya utekelezaji wa mradi huu katika maeneo hayo.

**Aidha,** Kamati ilibaini kuwa Mashine Humba iliyofungwa ina uwezo wa KV 200, ambao ni mkubwa ikilinganishwa na mahitaji ya eneo husika ambalo halina watumiaji wengi. Yapo maeneo mengine ambayo Kamati ilibaini kuwa yanahitaji Mashine Humba zenye uwezo mkubwa lakini zimefungiwa Mashine Humba zenye uwezo mdogo na hivyo kusababisha uharibikaji wa mara kwa mara.

### 2.1.1.3 Mradi wa Umeme wa Gesi Kinyerezi I Extension (MW 185) na Mradi wa Umeme wa Gesi wa Kinyerezi II (MW 240)

**Mheshimiwa Spika,** mradi huu unatekelezwa na Shirika la Umeme Tanzania (TANESCO) kwa lengo la kuzalisha MW 185 zaidi za umeme katika Mradi wa Umeme wa Gesi Kinyerezi I ambao tayari unazalisha MW 150. Mradi unakadiriwa kugharimu dola za kimarekani milioni 188 ambazo zimelipwa na

Serikali kwa asilimia mia moja (100%) na unatarajiwa kukamilika mwezi Juni, 2018.

Katika Mwaka wa Fedha 2016/2017, shilingi bilioni 110 zilitengwa na hadi wakati Kamati inakagua mradi huu, kiasi cha **shilingi bilioni 88** sawa na **asilimia 80%** kilikuwa kimeishatolewa katika utekelezaji wa mradi huo. Kamati inapongeza jitihada za Serikali kwa kupeleka fedha mapema katika mradi huo muhimu.

Pamoja na mafanikio hayo, Kamati ilibaini changamoto kadhaa zinazokabili utekelezaji wa mradi huu, ikiwa ni pamoja na tozo mbalimbali *(surcharges)* kutoka TANROADS na VAT zinazotokana na ukubwa na uzito usio wa kawaida wa mitambo inayotumika katika mradi huu (out of gauge heavy loads charges). Tozo hizo zinachangia kuongezeka kwa gharama za mradi na hivyo kuchelewesha utekelezaji wake.

**Mheshimiwa Spika, Pamoja na changamoto zinazoukabili mradi huu, bado dhamira ya dhati ya Serikali ya kuongeza kiwango cha upatikanaji wa umeme wa uhakika nchini kinazidi kudhihirika ambapo katika mwaka wa fedha 2017/2018 jumla ya shilingi bilioni 90 kutoka vyanzo vya ndani zimetengwa kwa ajili ya kuendeleza na kukamilisha mradi huu.**

**Mheshimiwa Spika, Kamati kupitia Bunge lako inaitaka Serikali kupeleka fedha zote za miradi ya umeme zilizobaki (Bakaa) kwa Mwaka wa fedha 2016/2017 ili kukamilisha miradi hiyo muhimu kwa wakati kama ilivyokusudiwa.**

**Mheshimiwa Spika,** Mradi wa Kinyerezi II MW 240 unatekelezwa na Shirika la Umeme Tanzania (TANESCO) kwa lengo la kuzalisha Megawati 240 kwa mfumo wa kisasa zaidi unaoitwa ***Combined Cycle Power Plant***. Gharama ya mradi huu ni dola za kimarekani milioni 344 ambapo asilimia themanini na tano (85%) ya gharama hizo italipwa na **Japan Export Trading Financing** na asilimia kumi na tano (15%) iliyobaki tayari imelipwa na Serikali ya Tanzania mwezi Februari, 2016.

Ujenzi wa Mradi huu umeishaanza na unatekelezwa kwa kasi, ambapo tayari misingi ya majengo imewekwa na baadhi ya mitambo kufungwa. Hata hivyo, pamoja na ujenzi huo kuanza kwa kasi, bado kuna changamoto mbalimbali za tozo kama vile forodha (*customs levies)*, railway levies, custom processing fees pamoja na *custom duties,* ambazo zinatakiwa kulipwa na TANESCO. Tozo hizo zimekuwa zikichangia ongezeko la gharama katika utekelezaji wa mradi huu.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati ilitaarifiwa kwamba, maombi ya TANESCO kwa TANROADS, ambayo yalihusu kupatiwa

msamaha wa kodi na tozo hizo zitokanazo na ukubwa na uzito wa mitambo usio wa kawaida (out of gauge heavy loads charges) yalikataliwa. Aidha, ucheleweshaji wa malipo hayo unaweza ukasababisha mitambo kuchelewa kufika eneo husika la mradi na hivyo kuchelewesha utekelezaji wa mradi.

### 2.1.1.4 Mradi wa Ukarabati wa Kituo cha Kufua Umeme Hale

**Mheshimiwa Spika**, Kamati ilifanya ziara ya ukaguzi katika Kituo cha Hale ambacho kilizinduliwa mwaka 1964. Kituo hiki ni moja ya vituo vitatu vinavyotumia nguvu ya maji kuzalisha umeme nchini, na kina mitambo miwili (2) yenye uwezo wa kuzalisha MW 10.5 kila mmoja. Mwaka 1986 mtambo mmoja ulipata hitilafu kwenye msuko wa Mashine Humba*(stator winding)*na ulifanyiwa marekebisho makubwa, hata hivyo, mtambo huo uliharibika tena mwaka 2004.

**Mheshimiwa Spika**, Serikali imeamua kufanya ukarabati mkubwa wa mitambo yote miwili kwa ufadhili wa Serikali ya Sweden, ambayo ilikubali kutoa Kroner Milioni 200 kupitia Shirika lake la misaada la SIDA. Asilimia 60 ya fedha hizo ni ufadhili na asilimia 40 ni Mkopo wa kibiashara. Makubaliano ya ufadhili wa mradi huu yalifanyika tarehe 11 Julai, 2013 baada ya upembuzi yakinifu kukamilika, hata hivyo ukarabati wa mitambo hiyo

bado haujaanza kwa kuwa bado hajapatikana mkandarasi atakaye tekeleza mradi huo.

Kamati inaona kwamba, kuchelewa kuanza kwa ukarabati wa Mitambo hiyo kunaendelea kupunguza zaidi Megawati 10 kwenye Gridi ya Taifa, hivyo Kamati inaishauri Wizara iharakishe taratibu hizo ili ukarabati uanze mapema kama ilivyokusudiwa.

#### 2.1.1.5 Mradi wa Bulyanhulu- Geita KV 220

**Mheshimiwa Spika,** Kamati ilitembelea mradi huu ambao unahusisha ujenzi wa kituo cha kupoza umeme cha Geita (msongo wa 220/33kv) pamoja na usambazaji wa umeme katika vijiji kumi (10) vilivyopo ndani ya eneo la utekelezaji wa mradi. Gharama za Mradi ni dola za kimarekani milioni 23 ambazo ni mkopo kutoka benki ya BADEA, na tayari gharama na fidia nyingine zote zimekwisha kukamilika na wananchi wote waliopisha eneo la mradi wameshalipwa fidia wanazostahili.

Pamoja na kukamilika kwa ulipaji fidia Wananchi waliopisha eneo la mradi, bado Mradi huu umeshindwa kuanza kwa wakati kutokana na kuchelewa kupatikana kwa Mhandisi Mshauri wa Mradi.

**Mheshimiwa Spika,** Mradi huu utakapoanza utasaidia kuongeza hali ya upatikanaji wa umeme wa uhakika katika Mkoa wa Geita. Aidha, Mradi huu utaunganisha wateja zaidi ya 1500 ukiwemo Mgodi wa Geita Gold Mine (GGM) ambao unahitaji zaidi ya MW 11 kwa ajili ya shughuli za Mgodi, na kusaidia Migodi mingine ya Wachimbaji wadogo ambayo haiendeshwi vizuri kutokana na kukosekana kwa umeme wa uhakika.

Kamati inaishauri Serikali kutatua changamoto hizo haraka iwezekavyo ili Mradi huo wenye tija kwa Mkoa wa Geita, uweze kuwanufaisha wananchi pamoja na wawekezaji wanaohitaji umeme mkubwa kwa ajili ya kuendesha shughuli zao.

**Mheshimiwa Spika, Kamati inaipongeza Serikali kupitia Wizara ya Nishati na Madini kwa kukamilisha mradi muhimu wa Rusumo Hydropower unaoziunganisha nchi tatu za Tanzania, Rwanda na Uganda, mradi huu umeongeza MW 26 kwenye Gridi ya Taifa. Mradi huu utasaidia upatikanaji wa umeme kwa mikoa ya Kagera na Kigoma na hivyo kupunguza matumizi ya umeme wa mafuta ambao ni ghali ukilinganisha na umeme wa maji.**

### 2.1.2 Miradi ya Sekta ya Madini iliyokaguliwa na Kamati

#### 2.1.2.1 Mgodi wa Dhahabu wa Buckleef

**Mheshimiwa Spika,** Mgodi wa Dhahabu wa Buckleef wenye leseni ya Uchimbaji Mkubwa(Special Mining License) SML Na. 04/92 uko katika Mkoa wa Geita na unamilikiwa kwa mkataba wa ubia ulioingiwa mwaka 2011 kati ya Serikali kupitia STAMICO na Kampuni ya TANZAM 2000.

**Mheshimiwa Spika,** kupitia mkataba huo, STAMICO inamiliki **asilimia 45** na TANZAM 2000 inamilki **asilimia 55** ya hisa. Kwa mujibu wa mkataba (Joint Venture Agreement) huo TANZAM 2000 ina jukumu la kutafuta fedha za kuendesha Mgodi (Operator) wakati jukumu la STAMICO lilikuwa kuhamishia Leseni zake 12 kwa Kampuni hiyo.

Hadi wakati wa ziara katika mgodi huu, Kamati ilibaini kwamba, licha ya Leseni zote za uchimbaji na utafiti kukabidhiwa kwa Kampuni hiyo, hakuna kazi yeyote iliyokwishafanyika katika kuendeleza Mgodi huo tangu Kampuni hiyo iingie Mkataba na STAMICO.

***Mheshimiwa Spika*****,** pamoja na Kampuni kuripoti kuwa imekamilisha ufungaji wa Mtambo mpya wa kuchenjulia dhahabu, Kamati inasikitishwa na kitendo cha mbia huyo

kutozingatia ushauri wa STAMICO kuhusu aina ya Mtambo unaofaa kutumika katika eneo hilo, hatua ambayo inaisababishia Serikali hasara. Kamati inaishauri Serikali kuwa makini inapoingia ubia katika Sekta ya madini ili kuepuka wabia wa aina hii ambao hawazingatii ushauri wa Mbia mwenza, (STAMICO) jambo linalosababisha hasara zisizo za msingi.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati haikuona jitihada zozote za Mbia huyo za kuendeleza Mgodi kama walivyokubaliana kwenye Mkabata. Aidha, Kamati imesikitishwa na usimamizi mbovu wa STAMICO katika Mgodi huo licha ya kuwa na Mashapo (Reverse) yenye uhakika wa kuzalisha Dhahabu na kuliingizia Taifa mapato. Aidha, hatua stahiki zichukuliwe ili kurekebisha kasoro ambazo zimebainika katika ubia huo.

#### 2.1.2.2 Migodi ya Wachimbaji Wadogo waliopata Ruzuku ya Serikali-Geita (Blueleef Mining na Mgusu Mining)

**Mheshimiwa Spika,** katika awamu zote mbili za malipo, jumla ya Shilingi Bilioni **8,071,000,000/=** zimetolewa na Serikali kwa kuratibiwa na Wizara ya Nishati na Madini, na jumla ya Wachimbaji Wadogo 115 wamenufaika kwa kupata ruzuku hizo katika mikoa mbalimbali. Katika awamu ya kwanza ya malipo, kiwango cha juu kwa kila mnufaika kilikuwa ni **Dola za**

**Kimarekani 50,000** na awamu ya pili kiwango cha juu cha mnufaika kilikuwa ni **Dola za Marekani 100,000.** Kwa maoni ya Kamati, viwango hivyo vya fedha ni vikubwa ikilinganishwa na usimamizi mdogo unaotolewa na Wizara ya Nishati na Madini.

Katika Mkoa wa Geita jumla ya Wachimbaji Wadogo Wadogo Saba (7 ) wamenufaika na ruzuku ya Serikali, vikiwemo Vikundi vya Wajasiriamali wanaoshughulika katika maeneo ya wachimbaji wadogo. Katika ziara ya ukaguzi wa Migodi ya wachimbaji wadogo waliopata ruzuku, Kamati iliridhishwa na utendaji wa wachimbaji wadogo watatu (3) tu kati ya Saba (7) waliopata ruzuku ambao wameendeleza shughuli zao za uchimbaji katika maeneo yao.

**Mheshimiwa Spika**, pamoja na mafanikio hayo kwa baadhi ya wanufaika, Kamati ilibaini changamoto kubwa ya usimamzi wa fedha usioridhisha kwa Wachimbaji Wadogo. Aidha, Wanufaika hao wa ruzuku kwa namna moja ama nyingine hawakutumia fedha hizo kwa malengo yaliyokusudiwa na Serikali.

Kwa kuwa, awamu zote mbili za utoaji wa ruzuku kwa Wachimbaji Wadogo kumekuwa na kasoro mbalimbali kwenye matumizi na usimamizi wa ruzuku hizo, Kamati inaishauri Serikali kufanya tathmini (evaluation) ya fedha hizo kabla haijaanza

awamu nyingine ili kuhakiki na kutatua changamoto nyingi ambazo zipo kwa sasa.

### 2.1.2.3 Migodi ya Wachimbaji wa Kati

**(Busolwa Mining na Nyarugusu Processing Plant)**

**Mheshimiwa Spika**, Kamati ilifanya ziara ya ukaguzi wa Migodi ya Busolwa Mining na Nyarugusu Processing Plant, iliyopo Mkoa wa Geita. Lengo la ziara lilikuwa ni kujifunza jinsi Wachimbaji wa Kati wanavyoendesha shughuli zao na kubaini mchango wao katika mapato ya Serikali.

Busolwa Mining ni Mgodi unaomilikiwa na Mtanzania, yaani mzawa kwa aslimia mia moja, na Kamati ilijionea jinsi unavyoendesha shughuli zake kwa kutekeleza Sheria na Kanuni mbalimbali, ikiwa ni pamoja na kulipa kodi zote za Serikali. Tangu Mgodi huo uanze kazi mwaka 2014, umeshalipa kodi za thamani ya **shilingi bilioni 120, Mrabaha shilingi Bilioni 562, kodi ya zuio kwa mwaka 2017 shilingi Milioni 20 na Service Levy shilingi Milioni 48.**

**Mheshimiwa Spika,**changamoto kubwa inayoukabili Mgodi huu ni ufinyu wa eneo hasa la kutupia mabaki yatokanayo na shughuli za Mgodi yaani (TSF). Hivyo ni mapendekezo ya Kamati kuwa, maombi ya Mgodi huo kupatiwa eneo lingine

yashughulikiwe mapema ili kusaidia kuongeza uhai wa Mgodi huo ambao umeajiri zaidi ya Watanzania 300.

## 3.0 SEKTA YA MADINI

### 3.1 Madini ya Vito ya Tanzanite

**Mheshimiwa Spika**, Kamati yako imeendelea kusikitishwa na jitihada ndogo zinazofanywa na Wizara ya Nishati na Madini za kuokoa mapato yatokanayo na Madini ya Vito yaani Tanzanite na Almasi nchini. Hata hivyo hakuna mikakati madhubuti ya kuokoa Rasimali hizi kutokana na usimamizi usioridhisha wa Migodi hiyo, pamoja na changamoto nyingi za Mikataba baina ya Stamico na Tanzanite One Mining Limited (TML), ambao ndiyo Mgodi pekee unaozalisha Madini haya Duniani.

**Mheshimiwa Spika,** Kampuni ya Tanzanite One Mining Limited (TML) amekuwa akitoa Taarifa za uongo kwa mbia mwenza yaani STAMICO toka alivyoanza uzalishaji wa Tanzanite hapa nchini, kwa mfano kuanzia Juni, 2013 hadi Machi, 2016 STAMICO ameripoti mauzo ya jumla ya **Dola za kimarekani Milioni 16,671,167** na TML katika kipindi hicho hicho aliuza Tanzanite yenye thamani ya **Dola za kimarekani Milioni 17,930,653** ambapo tofauti ya **Dola Milioni 1,259,483** hazikuripotiwa na Kampuni hiyo na hivyo hazikuripiwa kodi ya

Serikali. Hivyo, kutokana na tofauti hiyo Stamico wamepoteza jumla ya **Dola za kimarekani 182,855.19.**

**Mheshimiwa Spika,** pia kampuni hii ya Tanzanite One Mining Limited (TML) imekuwa hailipi kodi ya Mapato na tozo/gharama mbalimbali kwa Stamico kama vile Gharama ya Uangalizi na usimamizi (*Monitoring and Evaluation Unit Cost*) ambapo jumla ya **shilingi milioni 131,695,626** zinadaiwa na STAMICO, pia kukosekana kwa akaunti ya pamoja kati ya wabia hawa kuna sababisha mambo mengi hasa ya kifedha kutokufahamika kwa STAMICO kama inavyotakiwa na Mkataba (*Joint Venture*) huo.

**Mheshimiwa Spika,** kwa namna Mkataba huo unavyoendeshwa kwa pande hizi mbili (Joint Venture) umekuwa hauna manufaa kwa upande wa Serikali, kwa kuwa Kampuni hiyo imekuwa haitekelezi kwa kiasi kikubwa matakwa ya Mkataba huo pamoja na maagizo mbalimbali ya Serikali inayokuwa ikipewa hasa wakati Kampuni hiyo ilipofukuza Wafanyakazi zaidi ya 201 bila kufuata Sheria na utaratibu za nchi.

**Mheshimiwa Spika**, Tarehe 3 Mei, 2017, Kamati yako ilihudhuria maonesho ya madini ya Vito jijini Arusha, na kujionea jinsi maonesho haya yanavyoweza kuisaidia sekta hii ya Madini ya

Vito hapa nchini.  Pamoja na mafanikio ya kuanzisha Mnada na Maonesho hayo ya Vito hapa nchini, bado kuna changamoto nyingi zinazoikabili Sekta hii ya Madini ya Vito hasa kwa madini ya Tanzanite.

Changamoto kubwa ni utoroshawaji wa madini hayo nje ya nchi. Changamoto hiyo ndiyo inayoendelea kuliumiza Taifa letu kwa kuwa ndiyo nchi pekee Duniani yenye neema hiyo, nakuifanya Tanzania kuwa siyo nchi ya kwanza kwa uuzaji wa Madini hayo ya Vito duniani. Hata hivyo, uanzishwaji wa maonesho hayo kwa kiasi kikubwa bado haujaweza kusaidia kutatua changamoto zinazokabili sekta hii ya Madini ya vito hapa nchini.

**Mheshimiwa Spika,** pamoja na hasara kubwa tunayopata kama Taifa kwenye Madini haya pekee nchini, Kamati inalishauri Bunge lako tukufu kwa mara nyingine tena lifuatilie kwa kina changamoto za  Mkataba huo baina ya TML na STAMICO ili Bunge tuweze kuishauri Serikali namna bora ya kukabiliana na Mikataba isiyokuwa na maslahi kwa Taifa.

**Madini ya Dhahabu**

**Mheshimiwa Spika**, Sekta ya Madini nchini imeendelea kukabiliwa na changamoto nyingi hasa katika suala la ukusanyaji wa Kodi za Serikali. Sekta hii imekuwa ikichangia

asilimia 4% tu katika pato la Taifa, mchango ambao ni kidogo sana ikilinganishwa na ongezeko la uzalishaji katika Sekta hiyo.

Kwa mfano; katika mwaka 2016 nchi yetu ilizalisha jumla ya **Wakia milioni 1.42** za Madini ya Dhahabu ikilinganishwa na **Wakia milioni 1.36** zilizozalishwa katika mwaka 2015. Ongezeko hilo la uzalishaji ambalo ni sawa na **asilimia 4.4%,** lilitakiwa kwenda sambamba na ongezeko la ukusanyaji wa Kodi za Mapato nchini.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati inasikitishwa na ulipaji hafifu wa kodi za Mapato unaofanywa na Wawekezaji katika Migodi mikubwa hapa nchini.Kwa mfano; Mwaka 2016 ni Migodi miwili tu nchini ndiyo iliyolipa Kodi ya Mapato ambayo ni **North Mara Gold Mine na Geita Gold Mine.** Kamati inaitaka Serikali kuchukua hatua madhubuti juu ya Wawekezaji ambao hawalipi kodi ili kuhakikisha Kodi zote muhimu zinalipwa kwa wakati.

**Mheshimiwa Spika, kumekuwa na malalamiko mengi kutoka kwa Wawekezaji nchini hasa kwenye sekta ya Madini, wakiidai Serikali Kodi ya Ongezeko la Thamani (*VAT returns*) ambayo kiutaratibu inapaswa kulipwa baada ya Migodi kukamilisha hesabu zao na kuwasilisha TRA. Serikali haijalipa fedha hizo kwa Migodi hiyo kwa madai ya kuwepo changamoto kadhaa**

**ambazo Serikali ilikuwa inazifuatilia ili kujiridhisha kabla ya kuzilipa. Kamati inaishauri Serikali kutatua changamoto hizo ili Migodi hiyo iweze kulipwa fedha hizo.**

**Mheshimiwa Spika,** Serikali inamiliki mgodi mmoja tu kwa asilimia mia ambao ni Mgodi wa Stamigold kupitia Shirika la STAMICO. Mgodi huu licha ya kuajiri Watanzania zaidi ya mia saba (700), bado kumekuwa na jitihada ndogo za Serikali katika kuusaidia Mgodi huo katika masuala ya msingi ya kuuendeleza kama vile;

1. Serikali kutousaidia Mgodi kupata fedha za kufanya utafiti katika leseni zinazozunguka eneo hili ili kuongeza uhai wa mgodi;
2. Mgodi haujasaidiwa kupata msamaha wa kodi ya mafuta na vipuli vya uendeshaji kama ilivyo kwa migodi mingine ya wawekezaji nchini;
3. Ukosefu wa Mining Development Agreement (MDA) kwa muda mrefu unaukwamisha Mgodi kujiendesha kibiashara kama ilivyo kwa Migodi mingine nchini;
4. Mgodi huu unakabiliwa na deni kubwa kutoka kwa Wazabuni mbalimbali wanaotoa huduma katika Mgodi huo. Kamati inaitaka Serikali kuingilia kati deni hilo ili kuepusha shughuli za Mgodi huo kusimama na kusababisha hasara kubwa.

Kamati hairidhishwi na jitihada zilizofanywa na Serikali kupitia Wizara ya Nishati na Madini katika kuusaidia Mgodi huo wa Stamigold. Changamoto hizo zikitatuliwa kikamilifu, uzalishaji wa Madini ya Dhahabu unaweza kuongezeka katika Mgodi huo.

**Mheshimiwa Spika**, kumekuwa na malalamiko ya muda mrefu sasa kutoka kwa Wananchi wanaozunguka Mgodi wa North Mara hasa maeneo ya **Nyamichele** katika vijiji vya **Nyakunguru**, **Murwambe, Matongo** na **Nyamongo.** Pamoja na tathimini ya ardhi kukamilika toka mwezi Aprili, 2013 na Kamati kutoka Wizara ya Nishati na Madini, kukamilisha kazi yake ya tathmini na utatuzi wa changamoto hasa zile za mauaji katika eneo hilo,mpaka sasa Wananchi hao bado hawajalipwa fidia zao.

Kamati inashangazwa na hatua ya malipo ya Wananchi hao kucheleweshwa kwa takribani miaka minne sasa, licha ya Serikali kupitia Wizara ya Nishati na Madini, kuunda na kutuma Kamati za Uhakiki nne (4) kati ya mwaka 2014 hadi 2017.

Kamati inaishauri Serikali kuingilia kati suala hili, ili Wananchi hao ambao wameteseka kwa muda mrefu sasa waweze kupata stahiki zao.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati inampongeza Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. John Pombe Magufuli na kuunga mkono jitihada zake katika kuendelea kufuatilia kwa karibu zaidi Sekta hii ya Madini nchini, ikiwa ni pamoja na kuunda Kamati maalum ya Wataalamu iliyochunguza mchanga uliyo katika makontena ya mchanga wa madini (Makinikia)yaliyopo katika maeneo mbalimbali hapa nchini. Kamati hii iliweza kubaini uwepo wa viwango vingi vya madini ya dhahabu, shaba, silva, salfa, na chuma katika makinikia hayo yanayosafirishwa nje ya nchi.

Pia uchunguzi huo umeonesha kuwepo kwa madini ya kimkakati yaani *(Strategic metals) ambayo* niIridium, Rhodium, Ytterium, Beryllium, Tantalum na Lithium, madini haya kwa sasa yanahitajika sana Duniani na yana thamani kubwa sambamba na madini ya dhahabuambayo Taarifa zake zilikuwa hazitolewi na wawekezaji.

**Mheshimiwa Spika**, Hata hivyo, Kamati inaendelea kusubiri taarifa nyingine ya Kamati Maalum ya Waatalamu iliyoundwa na Mhe. Rais, inayoendelea na uchunguzi ambao utabainisha masuala ya Kiuchumi na Kisheria ili sasa kama Taifa tuweze kunufaika na Rasilimali zetu za Madini.

**Mheshimiwa Spika,** kwa dhati kabisa Kamati inakupongeza wewe binafsi kwa kuamua kufuatilia jambo hili kwa ukaribu, na kutoa uamuzi kuwa utaunda Kamati maalumu ya kufuatilia masuala ya Madini, ili Bunge lako tukufu nalo litekeleze kikamilifu jukumu lake la kikatiba la kuisimamia na kuishauri Serikali.

## 4.0 SEKTA NDOGO YA GESI.

**Mheshimiwa Spika,**tangu kugundulika kwa Gesi Asili nchini mwaka 1974 katika eneo la Songo Songo, mwaka 1982 katika eneo la Mnazi Bay pamoja na eneo la Bahari ya Kina kirefu mwaka 2010/12, uzalishaji wa gesi katika miradi yote iliyogundulika hapa nchini ulianza miaka ya 2004 hadi 2006.

Kamati inaipongeza Serikali kupitia Shirika la TPDC kwa kuandaa Mpango Kabambe wa Matumizi na Usambazaji wa Gesi Asilia nchini wa mwaka 2016-2045 **(Natural Gas Utilisation Master Plan).** Mpango huu utasaidia kwa kiasi kikubwa kutoa Dira ya Matumizi bora ya Gesi Asilia kwa kuzingatia vipaumbele mbalimbali vilivyowekwa ili Rasirimali hii iwafikie na kuwanufaisha Wananchi wengi.

**Mheshimiwa Spika,** pamoja na jitihada mbalimbali zinazofanywa na **TPDC,** bado kuna changamoto kubwa ya Madeni yanayolikwamisha Shirika hili katika uendelezaji wa

miradi yake. Madeni hayo yanasababishwa na hatua ya Serikali kutenga fedha kidogo kwenye miradi hiyo muhimu na hivyo kukwamisha Shirika kutekeleza miradi hiyo kwa wakati.

**Mheshimiwa Spika,** tangu kugundulika kwa Gesi hiyo hapa nchini, jumla ya Viwanda 41 na Taasisi 2 vimekwisha unganishwa katika mtandao wa matumizi ya Gesi Asilia. Aidha, Kamati inaipongeza Serikali kwa kuendeleza miradi ya kuzalisha umeme kwa kutumia Gesi Asilia. Miradi hiyo mikubwa inatarajiwa kukamilika ifikapo Juni, 2018 ambapo inatarajiwa kuongeza zaidi ya Megawati 425 kwenye Gridi ya Taifa, na hivyo kupunguza tatizo la umeme nchini**.**

## 2.3 Maoni ya Jumla kuhusu Utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo kwa mwaka wa Fedha 2016/2017

**Mheshimiwa Spika,** kutokana na ziara ya ukaguzi wa miradi ya maendeleo Kamati inatoa maoni yafuatayo:-

i) Utekelezaji wa Bajeti kwa Wizara ya Nishati na Madini, haukuwa wa kuridhisha kwa kuwa fedha iliyotolewa hadi Machi, 2017 ni asilimia 36 tu;

ii) Miradi mingi haikutekelezeka kama ilivyopangwa kwa kuwa fedha zilizotengwa hazikutolewa na kupelekwa kwa wakati kama ilivyotakiwa;

iii) Miradi mingi ya REA katika Awamu ya Pili haikukamilika kutokana na kasoro mbalimbali kama vile uainishaji wa maeneo bila kuzingatia vijiji na vitongoji ambavyo tayari vina wananchi wengi, na ufungaji wa Mashine Humba nyingi kutokidhi mahitaji ya eneo husika;

iv) Serikali iangalie upya namna bora ya kuwasaidia **Wachimbaji wa Kati** kwa kuwapatia maeneo ya kutosha kwa kuwa wameonesha nia ya dhati ya kuendeleza Sekta ya Madini;

v) Ruzuku iliyotolewa na Serikali kupitia Wizara ya Nishati na Madini kwa Wachimbaji Wadogo Wadogo, haikusimamiwa vizuri na hivyo kushindwa kuleta tija kwa Wananchi waliokusudiwa;

vi) Pamoja na Mipango mizuri ya TPDC katika kuendeleza Sekta ya Gesi nchini, ni lazima Serikali iwekeze fedha za kutosha katika miradi ya Gesi ili kuharakisha azma ya nchi yetu kuingia katika uchumi wa viwanda;

vii) Serikali itenge fedha za kutosha na kuzipeleka kwa wakati kwenye miradi ya kimkakati kama vile Mgodi wa makaa ya Mawe wa Kiwira; na

viii) Uwekezaji katika sekta ya madini unahitaji kuangaliwa upya hasa katika uwekezaji wa Migodi mikubwa.

## 3.0 UCHAMBUZI WA TAARIFA YA UTEKELEZAJI WA BAJETI NA UZINGATIAJI WA MAONI YA KAMATI KWA MWAKA WA FEDHA 2016/2017


**Mheshimiwa Spika**, Kamati ilifanya uchambuzi wa Bajeti kwa kuzingatia mambo makuu matatu ambayo ni:- Makusanyo ya Maduhuli kwa mwaka wa fedha 2016/2017, Hali ya upatikanaji wa fedha kutoka Hazina na Uzingatiaji wa maoni na ushauri uliotolewa na Kamati ya Nishati na Madini wakati huo.

### 3.1 Uchambuzi wa Taarifa kuhusu Ukusanyaji wa Maduhuli kwa mwaka wa fedha 2016/2017

**Mheshimiwa Spika**, Wizara ilipanga kukusanya maduhuli yenye jumla ya Shilingi bilioni **370.68** ikilinganishwa na **Shilingi bilioni 286.66** kwa mwaka wa fedha 2016/2017. Taarifa ya utekelezaji inaonesha kuwa, hadi kufikia 28 Februari, 2017, Wizara ilikuwa imekusanya jumla ya **Shilingi bilioni 239.38** sawa na **asilimia 64.5** ya lengo. Makusanyo hayo yanaweza kufikia lengo lililowekwa kama Wizara itaongeza juhudi katika kipindi kilichobaki.

Uchambuzi wa Kamati umebaini kuwa Makadirio ya mchango wa Idara ya Madini kwa mwaka fedha 2017/18 yameshuka kwa asilimia **4.5%** ikilinganishwa na mwaka wa fedha 2016/17. Aidha, Makadirio ya mchango wa Idara ya Nishati, yameongezeka kwa asilimia **4.5%** katika mwaka wa fedha 2017/18 ikilinganishwa na mwaka wa fedha 2016/17. Ufafanuzi zaidi umeoneshwa kupitia Kielelezo Na. 01 cha Taarifa hii.

**Kielelezo Na. 01**




| | 2016/2017 KIASI | 2016/2017 ASILIMIA | 2017/2018 KIASI | 2017/2018 ASILIMIA |
|---|---|---|---|---|
| IDARA YA MADINI | 215,962,385,000 | 58.3 | 194,397,889,999 | 53.8 |
| IDARA YA NISHATI | 154,377,501,000 | 41.6 | 166,326,844,600 | 46.1 |
| IDARA NA VITENGO VINGINE | 344,003,000 | 0.1 | 266,403,000 | 0.1 |

Aidha Kamati ilielezwa sababu zilizosababisha kuongezeka kwa makusanyo kwa Mwaka wa Fedha 2016/2017 kama ifuatavyo:-

i) Usimamizi bora wa mapato kutoka vyanzo vya ndani;

ii) Kuanzishwa kwa Minada ya Madini ya Vito nchini;

iii) Kuongezeka kwa Mauzo ya Gesi Asilia kwa watumiaji wapya hasa baada ya viwanda vipya zaidi ya 41 kuunganishwa kwenye mtandao wa matumizi ya Gesi;

## 3.2 Upatikanaji wa Fedha kutoka Hazina

**Mheshimiwa Spika**, kwa Mwaka wa Fedha 2016/2017 Wizara ya Nishati na Madini iliidhinishiwa jumla ya **Shilingi trilioni 1.12** kwa ajili ya kutekeleza majukumu yake. Hadi kufikia tarehe 13 Machi, 2017 Wizara ilikuwa imepokea jumla ya **Shilingi Bilioni 404.12,** sawa na asilimia 36 ya Bajeti yote iliyoidhinishwa na Bunge lako tukufu.

Bajeti ya Miradi ya Maendeleo iliyoidhinishwa na Bunge lako ilikuwa ni **Shilingi Trilioni 1.06,** sawa na **asilimia 94** ya bajeti yote ya Wizara kwa mwaka wa fedha 2016/17. Hadi kufikia Machi, 2017 **Shilingi Bilioni 372.88** zilikuwa zimetolewa, sawa na **asilimia 35 tu** ya fedha za Maendeleo.

Kwa upande wa fedha za Matumizi Mengineyo (OC), fedha iliyoidhinishwa ilikuwa **Shilingi bilioni 66.22** na hadi kufikia Machi, 2017 Wizara ilikuwa imepokea kiasi cha **Shilingi Bilioni 31.24**, sawa na **asilimia 47**% ya fedha zilizoidhinishwa. Mwenendo huu wautolewaji wa fedha za matumizi mengineyo

unakwamisha usimamizi bora wa fedha za miradi ya maendeleo, kwani Watendaji wanashindwa kusimamia miradi hiyo kwa kukosa fedha.

**Mheshimiwa Spika,** Bajeti ya fedha za maendeleo kutoka nje kwa mwaka wa fedha 2016/17 ilikuwa ni **Shilingi Bilioni 331.51**. Hadi kufikia Machi, 2017jumla ya S**hilingi Bilioni 38.57**, sawa na **asilimia 12%** tu zilipokelewa na kupelekwa katika miradi mitatu ambayo ni Miradi ya Umeme Vijijini, Mradi wa Hale Hydropower na Mradi wa Makambako- Songea**.** Upatikanaji huu mdogo wa fedha za nje kwenye miradi ya Maendeleo, umekwamisha kwa kiasi kikubwa utekelezaji wa miradi mingi iliyotengewa kiasi kikubwa cha fedha za nje.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati inaipongeza Wizara ya Nishati na Madini kwa kubaini namna utegemezi wa fedha za nje za maendeleo unavyoathiri utekelezaji wa miradi hiyo, na hivyo kuamua katika Bajeti ya Mwaka wa fedha 2017/18 kutenga fedha za maendeleo kutoka vyanzo vya ndani tu. Uamuzi huu utasaidia miradi mingi kutekelezwa bila kutegemea fedha za Wahisani ambao wamekuwa hawatekelezi kikamilifu ahadi zao.

Ufafanuzi zaidi kuhusu uwiano kati ya Bajeti iliyoidhinishwa na fedha zilizopatikana hadi Machi, 2017 ni kama unavyoonekana kupitia Kielelezo No.2 katika taarifa hii.

**Kielelezo Na. 2**

| **BAJETI ILIYOIDHINISHWA 2016/2017** | | | **FEDHA ILIYOPATIKANA HADI MACHI,2017** | |
|---|---|---|---|---|
| **UFAFANUZI** | **KIASI** | **ASILIMIA** | **KIASI** | **ASILIMIA** |
| **JUMLA KUU** | Tri 1.12 | 100 | Bil 404.12 | 36 |
| **FEDHA ZA MAENDELEO** | Tri 1.06 | 94 | Bil 372.88 | 35 |
| **MATUMIZI YA KAWAIDA** | Bil 66.22 | 6 | Bil 31.24 | 47 |

***CHANZO:*** *Taarifa ya Wizara ya Nishati na Madini Fungu 58 kuhusu utekelezaji wa bajeti kwa mwaka wa fedha 2016/17*.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati inasikitishwa na utolewaji wa fedha za miradi ya maendeleo usioridhisha, hivyo kusababisha miradi mingi kushindwa kukamilika kama ilivyopangwa katika mwaka wa fedha 2016/17. Kamati inaona ni vyema kuwa na miradi michache ya kipaumbele ambayo itaweza kupelekewa fedha kuliko kuwa na miradi mingi ambayo haitaweza kutekelezwa kwa mwaka husika kwa kukosa fedha.

### 3.3 Mapitio ya Utekelezaji wa Ushauri wa Kamati

**Mheshimiwa Spika**, katika uchambuzi wa Bajeti ya Mwaka 2016/17, Kamati ilitoa Maoni, Ushauri na Mapendekezo, kwa kuzingatia matakwa ya Kanuni ya 7(1) ya Nyongeza ya Nane ya Toleo la Januari, 2016 iliyoelezea majukumu ya Kamati ya kusimamia na kufuatilia utendaji kazi wa shughuli za Wizara katika Sekta za Madini na Nishati. Napenda kuliarifu Bunge lako tukufu kuwa, baadhi ya ushauri uliotolewa na Kamati umezingatiwa na baadhi bado haujafanyiwa kazi na Serikali kama ifuatavyo:-

**Mheshimiwa Spika**, bado kuna tatizo la usimamizi usioridhisha katika miradi ya Umeme Vijijini, katika maeneo mengi hapa nchini. Katika ziara ya ukaguzi wa miradi ya maendeleo, Kamati ilibaini changamoto mbalimbali katika maeneo mengi zilizoathiri utekelezaji wa miradi. Mfano; ufungaji wa Mashine Humba zilizochini ya kiwango katika maeneo mengi umesababisha kuharibika mara kwa mara na hivyo wananchi waliopata miradi ya umeme vijijini kutokupata faida ya Nishati hiyo hata baada ya kukamilika kwa miradi hiyo.

Fedha zilizotengwa kwa ajili ya baadhi ya miradi ya kimkakati ni kidogo sana ukilinganisha na mahitaji halisi ya fedha zinazohitajika katika kuendeleza miradi hiyo. Kamati haioni dhamira ya dhati ya Serikali ya kuendeleza miradi hiyo, hasa ile

ya Joto Ardhi ambayo utekelezaji wake haujaanza licha ya upembuzi yakinifu kukamilika muda mrefu uliopita.

**Mheshimiwa Spika,** kuhusu jitihada zinazofanywa na Serikali za kulipa madeni ya TANESCO, Kamati haioni mikakati ya dhati ya Serikali ya kumaliza madeni hayo kwa wakati. Aidha, mwenendo hafifu wa ulipaji wa madeni hayo unakwamisha kwa kiasi kikubwa shughuli za utendaji wa Shirika hilo.

## 4.0 UCHAMBUZI WA MPANGO NA MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI KWA (FUNGU 58) MWAKA WA FEDHA 2017/2018

### 4.1 Mapitio ya Malengo ya Wizara kwa Mwaka wa Fedha 2017/2018

**Mheshimiwa Spika**, wakati wa kufanya uchambuzi wa Makadirio ya Bajeti kwa Mwaka wa Fedha 2017/18, Kamati imebaini kuwa Wizara imekuwa ikisimamia na kutekeleza malengo hayo zaidi ya miaka mitano sasa. Hii inatokana na umuhimu wake kwa kuzingatia majukumu yaliyoainishwa kwa mujibu wa Sheria ya Utekelezaji wa Majukumu ya Wizara ya Nishati na Madini, Sura 299, The Ministers (Discharge of the Ministerial Functions) Act.

**Mheshimiwa Spika,** Mwaka wa Fedha 2017/18 Wizara itatekeleza na kusimamia Malengo Makuu Matano (5) yafuatayo:-

i) Kuimarisha usimamizi na uendelezaji wa Sekta ya Nishati kwa Maendeleo endelevu ya Taifa;
ii) Kuboresha uendelezaji na usimamizi endelevu wa rasilimali za madini kwa maendeleo ya kijamii na kiuchumi;
iii) Kuimarisha utoaji wa huduma kwa wadau katika Sekta za Nishati na Madini;
iv) Kuboresha utoaji wa huduma kwa watumishi waathirika wa VVU na UKIMWI ili kupunguza maambukizi; na
v) Kuondoa vitendo vya rushwa katika sekta ya Nishati na Madini.

**Mheshimiwa Spika,** malengo haya yakitekelezwa vizuri yatatimiza azma ya Wizara ya kuendeleza sekta inazozisimamia hasa Sekta ya Madini ambayo inatarajiwa kuongeza pato la Taifa, na Sekta ya Nishati inayotegemewa kutekeleza azma ya Taifa kufikia Uchumi wa Viwanda unaotarajiwa na Wananchi wetu.

## 4.2 Uchambuzi wa Makadirio ya Mapato

**Mheshimiwa Spika,** Mwaka wa Fedha 2017/18 Makisio ya makusanyo ya Maduhuli yanakadiriwa kuwa jumla ya **Shilingi bilioni 360.99** ikilinganishwa na **Shilingi bilioni 370.68** kwa mwaka wa fedha 2016/17. Kati ya makusanyo hayo **Shilingi**

**bilioni 194.39** sawa na **asilimia 53.8** zitakusanywa na Idara ya Madini, **Shilingi bilioni 166.33** sawa na **asilimia 46.6%** zitakusanywa na Idara ya Nishati na **Shilingi bilioni 266.40** sawa na **asilimia 0.1%** zitakusanywa na Idara na Vitengo vingine katika Wizara.

Makadirio ya makusanyo ya mapato yameshuka kwa **asilimia 2.6%** ikilinganishwa na makadirio ya makusanyo ya mwaka wa fedha 2016/17. Aidha Makusanyo ya maduhuli kwa Idara ya Madini yameshuka kwa **asilimia 9.98%** ikilinganishwa na makusanyo ya Mwaka wa fedha 2016/17.

**Kamati inataka kufahamu ni kwa sababu gani Makusanyo ya Maduhuli kwa Idara ya Madini yanatarajiwa kushuka ilhali kama nchi tunatamani Sekta ya Madini iendelee kutoa mchango mkubwa kwenye pato la Taifa**.

## 4.3 Uchambuzi wa Makadirio ya Matumizi

**Mheshimiwa Spika**, makadirio ya matumizi ya Bajeti ya Wizara ya Nishati na Madini kwa mwaka wa fedha 2017/2018 ni jumla ya **Shilingi Bilioni 998,337,759,500** ikilinganishwa na **Shilingi Trilioni 1,122,845,741,000** zilizoidhinishwa na Bunge kwa mwaka 2016/2017. Bajeti hii ya Matumizi imepungua kwa **asilimia 11.1%**.

Kamati ilitaka ufafanuzi ni kwanini Bajeti hii imeshuka kwa kiwango hicho, wakati nchi inatarajia kuendeleza miradi mikubwa ya Nishati ambayo inategemewa katika uchumi wa Viwanda. Wizara ilifafanua kuwa Bajeti hii imeshuka kutokana na kupungua kwa fedha za nje hasa kwenye Miradi ya Maendeleo.

Kamati inaishauri Wizara kuacha kutegemea sana fedha za nje, kwa kuwa zimekuwa hazitolewi kwa wakati na hivyo kuathiri kwa kiasi kikubwa utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo kwa mwaka husika**.** Kwa mfano; Bajeti ya nje kwa mwaka wa fedha 2016/17 ilikuwa **Shilingi Bilioni 331.51.** Hadi kufikia Machi, 2017 Wizara ilikuwa imepokea **Shilingi Bilioni 38.57** sawa na **asilimia 12%** ya Bajeti yote iliyotegemewa katika miradi ya maendeleo.

Fedha za ndani kwa ajili ya REA zimepungua kutoka **Shilingi Bilioni 534,400,000,000** mwaka 2016/17 hadi **Shilingi Bilioni 469,090,426,000** kwa mwaka 2017/18, upungufu ambao ni sawa na **asilimia 12.2%.** Aidha, bajeti hii itatoka kwenye tozo mbalimbali, ambapo tozo za mafuta ni **Shilingi 354,950,000,000** na tozo ya Umeme ni **Shilingi 41,514,000,000** na Bajeti ya Serikali ni **Shilingi 72,626,426,000**.

**Mheshimiwa Spika,** kupungua kwa Bajeti ya Miradi ya Maendeleo pamoja na mwenendo wa upatikanaji wa fedha za Miradi ya maendeleo usioridhisha, kama ilivyoshuhudiwa kwa mwaka wa fedha 2016/17, kunaweza kusababisha miradi mingi ya kimkakati kushindwa kutekelezwa kama ilivyokusudiwa.

Aidha, bajeti ya matumizi ya kawaida kwa mwaka wa fedha 2017/18 ni **Shilingi Bilioni 59,705,753,500.** Bajeti hii imepungua kwa **asilimia 10.2%** ikilinganishwa na bajeti ya mwaka wa fedha 2016/17 ambayo ilikuwa **Shilingi Bilioni 66,481,072,000.** Kati ya fedha hizo **Shilingi Bilioni 28,833,681,500** ni kwa ajili ya matumizi mengineyo (OC), ambazo pia zimepungua ikilinganishwa na **shilingi Bilioni 38,654,138,000** zilizotengwa mwaka 2016/17.

Kuendelea kupungua huku kwa bajeti ya Matumizi ya Kawaida kunaweza kupunguza ufanisi katika kusimamia Bajeti ya Miradi ya Maendeleo iliyotengwa kwa Watumishi kukosa fedha za kwenda kusimamia Wakandarasi wanaotekeleza miradi hasa ile ya Umeme Vijijini.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati yako hairidhishwi na utekelezaji wa Bajeti ya Wizara inayoidhinishwa na Bunge lako tukufu, kutokana na kiasi cha fedha kinachotolewa kuwa kidogo. Kwa

mfano; kwa upande wa bajeti ya maendeleo, fedha zinazoidhishwa na Bunge, na kiasi ambacho kimekuwa kikitolewa ni chini ya asilimia 50.

Mwenendo huo wa Bajeti hauwezi kuleta tija kwenye utekelezaji wa miradi inayokusudiwa katika kipindi husika. Ni vyema Serikali ikatenga Bajeti inayotekelezeka kwa kuanisha miradi michache na kuhakikisha fedha za utekelezaji wake zinapelekwa kikamilifu.

## 5.0 MAONI NA USHAURI WA KAMATI

**Mheshimiwa Spika**, baada ya Kamati kutekeleza majukumu yake ya kikanuni ambayo ni ukaguzi wa miradi ya maendeleo, uchambuzi wa Taarifa ya Utekelezaji wa Bajeti ya Wizara, kwa mwaka wa fedha 2016/17 na makadirio na matumizi ya Wizara kwa mwaka wa fedha 2017/18, Kamati ina maoni na ushauri ufuataoa:-

5.1 Kwa kuwa, utekelezaji wa Miradi ya Umeme vijijini katika awamu mbili zilizokamilika ulikuwa na changamoto nyingi hasa katika Mikoa ya Tanga na Geita,ambako Kamati ilitembelea na kukagua; Kamati inashauri kuwa,changamoto zilizobainika ikiwa ni pamoja na baadhi ya maeneo kurukwa, zipatiwe ufumbuzi wa

haraka kabla ya kuendelea kwa Mradi wa Umeme vijijini,Awamu ya Tatu (REA III) .

5.2 Kamati inaishauri Serikali ikamilishe taratibu za kumaliza changomoto zilizojitokeza na kuchelewesha malipo ya Kodi ya Ongezeko la Thamani (VAT returns) kwa wawekezaji wa sekta ya Madini ili kuendelea kuboresha hali ya uwekezaji hapa nchini.

5.3 Pamoja na juhudi mbalimbali zinazofanywa na Wizara katika usimamizi wa Madini ya Tanzanite, Kamati inashauri Serikali kuwa, iangalie upya Mikataba yote iliyoingiwa na STAMICO na mbia mwenza kama ina tija kwa Taifa.

5.4 Ruzuku kwa Wachimbaji Wadogo iliyotolewa na Serikali katika awamu zote mbili kwa kiasi kikubwa imeshindwa kutimiza malengo kwa kukosa usimamizi mzuri. Aidha, ni vema Serikali kupitia Wizara ya Nishati na Madini ikaangalia namna bora ya kusimamia fedha hizi ikiwa ni pamoja na kuwapatia mafunzo Wachimbaji na kufuatilia kwa karibu shughuli za Wachimbaji hao.

5.5 Sekta ya Uchimbaji wa Kati imeendelea kukua kwa kiasi cha kuridhisha, hivyo ni vyema Serikali ikaangalia upya jinsi ya kuisaidia kupata baadhi ya misamaha ya kodi

kwenye Mafuta na Vipuli vinavyotumika katika shughuli za uchimbaji nchini.

5.6 Leseni zote ambazo zinakiuka Sheria ya Madini ikiwa ni pamoja na kushindwa kuendelezwa kwa muda mrefu, zifutwe na kupewa Wachimbaji Wadogo na wa Kati, kwa kuwa wameonesha nia ya dhati ya kuendeleza Sekta hiyo nchini.

5.7 Pamoja na Serikali kuandaa Mpango Kambambe wa Matumizi ya Gesi Asilia nchini, ni vyema ukafanyika utafiti na upembuzi yakinifu kuhusu miradi yote mikubwa ya usambazaji wa Gesi katika maeneo mbalimbali, ili kuweza kujua kama ina manufaa ya kiuchumi (***Economic Value****)*kwa Taifa. Hatua hii itasaidia kuepusha nchi kujiingiza kwenye mikopo ambayo ni mzigo kwa Taifa.

## 6.0 HITIMISHO

**Mheshimiwa Spika,** nichukue fursa hii kukupongeza wewe binafsi, Naibu Spika na Wenyeviti wote wa Bunge, kwa kazi nzuri mnayoifanya ya kuliongoza Bunge. Mungu awajalie afya njema, hekima na busara, katika kutekeleza wajibu huu mkubwa tuliowakabidhi**.**

Napenda kutoa shukrani zangu za dhati kwa niaba ya Wajumbe wa Kamati ya Kudumu ya Nishati na Madini, kwa Mhe. Prof. Sospeter Mhongo, (Mb) - aliyekuwa Waziri wa Nishati na Madini, Mhe. Dkt. Merdad Kalemani, (Mb)- Naibu Waziri wa Nishati na Madini, pamoja na Watendaji wote wa Wizara hiyo wakiongozwa na Kaimu Katibu Mkuu, Prof. James Mdoe, kwa ushirikiano wao mkubwa kwa Kamati yetu wakati wote.

Kwa namna ya pekee nawashukuru Wajumbe wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Nishati na Madini, kwa mchango wao adhimu katika shughuli za Kamati, katika kipindi hiki cha uchambuzi wa Bajeti kwa Fungu 58. Ni dhahiri shahiri kuwa, bila weledi na ushirikiano walionipa, Kamati isingeweza kufikia hatua hii ya mafaniko.

Kwa heshima kubwa naomba majina yao katika orodha ifuatayo yaingizwe kwenye Hansard:-

1. Mhe. Doto Mashaka Biteko, Mb - Mwenyekiti
2. Mhe. Deogratius Ngalawa, Mb - M/Mwenyekiti
3. Mhe. Mohamed Juma Khatib, Mb - Mjumbe
4. Mhe. Ally Mohamed Keissy, Mb - “
5. Mhe. Yussuf Kaiza Makame, Mb - “
6. Mhe. Zainabu Mussa Bakar, Mb - “
7. Mhe. Haroon Mulla Pirmohamed, Mb - “
8. Mhe. Mwantakaje Haji Juma, Mb - “

9. Mhe. Daimu Iddi Mpakate, Mb - “
10. Mhe. Catherine Valentine Magige, Mb - “
11. Mhe. Oscar Rwegasira Mukasa, Mb - “
12. Mhe. Stella Ikupa Alex, Mb - “
13. Mhe. Joyce Bitta Sokombi, Mb - “
14. Mhe. Bahati Ali Abeid, Mb - “
15. Mhe. Mauled Said Abdalah Mtulia, Mb - “
16. Mhe. Desderius John Mipata, Mb - “
17. Mhe. Katani Ahmad Katani, Mb - “
18. Mhe. Susan Limbweni Kiwanga,Mb - “
19. Mhe. Vedastus Mathayo Manyinyi, Mb - “
20. Mhe. Bupe Nelson Mwakang'ata, Mb - “
21. Mhe. Maryam Salum Msabaha, Mb - “
22. Mhe. Innocent Lugha Bashungwa,Mb - “
23. Mhe. Wilfred Muganyizi Lwakatare, Mb - “
24. Mhe. Dunstan Luka Kitandula, Mb - “
25. Mhe. John Wegesa Heche, Mb - “
26. Mhe. Anne Kilango Malecela, Mb - “

**Mheshimiwa Spika,** kwa namna ya pekee napenda kumshukuru Katibu wa Bunge, Dkt. Thomas Didimu Kashilillah, Mkurugenzi wa Idara ya Kamati za Bunge, Ndg. Athuman Hussein, Mkurugenzi Msaidizi, Ndg. Michael Chikokoto, Makatibu wa Kamati Ndg. Mwanahamisi Munkunda na Ndg. Felister Mgonja, pamoja na Msaidizi wa Kamati, ndg.

Kokuwaisa Gondo, kwa uratibu mzuri wa shughuli zote za Kamati na hatimaye kukamilisha Taarifa hii kwa wakati.

Naomba sasa Bunge lako Tukufu, likubali kuidhinisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya **Fungu 58** kwa Mwaka wa Fedha 2017/2018 ambayo ni **Shilingi 998,337,759,500.**

**Mheshimiwa Spika,** naunga mkono hoja na naomba kuwasilisha.

Dotto Mashaka Biteko, (Mb)
**MWENYEKITI**
**KAMATI YA BUNGE YA NISHATI NA MADINI**
01Juni, 2017